JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA TANZANIA

# HOTUBA YA JAJI MKUU WA TANZANIA MHE. PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA, SIKU YA SHERIA TANZANIA MWAKA 2025 TAREHE 03 FEBRUARI, 2025 DODOMA – TANZANIA

**KAULI-MBIU:**

**"TANZANIA YA 2050: NAFASI YA TAASISI ZINAZOSIMAMIA HAKI-MADAI KATIKA KUFIKIA MALENGO MAKUU YA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO."**



# HOTUBA YA JAJI MKUU MHE. PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA, SIKU YA SHERIA TANZANIA MWAKA 2025 TAREHE 03 FEBRUARI, 2025 DODOMA – TANZANIA

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**

**Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani,**

**Wahe. Majaji wa Mahakama ya Rufani,**

**Mhe. Khamis Ramadhan Abdalla, Jaji Mkuu wa Zanzibar,**

**Mhe. Mohamed Chande Othman, Jaji Mkuu Mstaafu,**

**Mhe. Jaji Nestor Kayobera, Rais wa Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki,**

**Mhe. Dkt. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi,**

**Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria,**

**Mhe. Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma,**

**Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu,**

**Mhe. Hamza Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali,**

**Wahe. Majaji wa Rufani Wastaafu, Majaji Kiongozi Wastaafu, na Majaji wa Mahakama Kuu Wastaafu,**

**Wahe. Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Mahakama,**

**Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania,**

**Mhe. Eva Kiaki Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania,**

**Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama,**

**Bw. Boniface Mwabukusi, Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika,**

**Wahe. Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa, Wasajili, Naibu Wasajili, Wakurugenzi na Watendaji wa Mahakama, Mahakimu na Mawakili,**

**Vingozi wa Vyama vya Siasa,**

**Viongozi wa Dini,**

**Ndugu Wanahabari,**

**Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana.**

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!***

***Mahakama ya Tanzania***

## 1. UTANGULIZI

**Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano,**

Awali ya yote, ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana tena katika siku hii muhimu kwa Mahakama ya Tanzania na wadau wa sheria nchini tukiwa na afya njema. Kwa niaba ya Mahakama ya Tanzania, ninatoa shukrani za dhati kwako kwa kukubali mwaliko wangu wa kuwa Mgeni Rasmi pamoja na ukweli kwamba una majukumu mengi ya kitaifa, hususani ikizingatiwa aina ya mwaka tulionao kisiasa.

**Mheshimiwa Rais,** Maadhimisho ya Siku ya Sheria Tanzania, mbali na kuashiria kuanza kwa mwaka mpya wa kazi wa mahakama, yamekuwa yakitumika kufikisha maombi kwa Mwenyezi Mungu na kuwaombea watoaji haki na kuwakumbusha kuwa kazi ya utoaji haki ni ya Mwenyezi Mungu na sisi ni mawakala tu wa kutimiza wajibu huu.

**Mheshimiwa Rais,** wapo Waheshimiwa Majaji, Mahakimu, Watumishi, na Wadau wengine wa Mahakama ambao

tulikuwa nao mwaka uliopita kwenye shughuli kama hii lakini, kwa masikitiko makubwa, sasa wametangulia mbele za haki. Ikikupendeza, ninakuomba tusimame kwa dakika moja ili tuwakumbuke na tuwaombee.

**Mheshimiwa Rais,** imekuwa utamaduni wetu kwamba, Maadhimisho ya Siku ya Sheria hutanguliwa na **Wiki ya Sheria,** ambayo hutumika kutoa elimu kwa umma ikiwemo kuwasikiliza wananchi ambao hutoa mrejesho na maoni kuhusu utoaji haki nchini. Kwa mwaka huu, wiki hiyo ya utoaji elimu ilizinduliwa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 25 Januari kwenye Viwanja vya Mwalimu Nyerere, Jijini Dodoma.

**Mheshimiwa Rais,** wananchi waliopata elimu wametoa maoni mbalimbali ambayo kwetu ni mtaji wa kutusaidia kujipima na kuweka mikakati thabiti ya kuboresha huduma za utoaji haki nchini. Tunaendelea kuboresha huduma za utoaji haki tukiamini kuwa huduma bora huchangia utulivu, amani, na umoja unaowezesha kufikiwa kwa mipango mbalimbali ya maendeleo kwa mtu mmojammoja, familia, na taifa kwa ujumla.

## 2. KAULI-MBIU MWAKA 2025

**Mheshimiwa Rais,** Mahakama ya Tanzania kama chombo cha utoaji haki ina mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Kwa kutambua kuwa taifa lipo katika umaliziaji wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 na maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050, kaulimbiu ya Siku ya Sheria Tanzania mwaka huu inaakisi dira hiyo na kuhimiza taasisi za haki-madai nchini kushiriki kikamilifu kuwezesha kufikiwa kwa malengo na matarajio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050. Hivyo, Maadhimisho ya Wiki na Siku ya Sheria yameongozwa na kaulimbiu isemayo **"TANZANIA YA 2050: NAFASI YA TAASISI ZINAZOSIMAMIA HAKIMADAI KATIKA KUFIKIA MALENGO YA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO".**

**Mheshimiwa Rais,** tunatambua kuwa mipango ya maendeleo ya nchi imekuwa ikiongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 iliyoanza kutumika mwaka 2000. Katika kutimiza lengo la Dira hiyo, mahakama imeimarisha mfumo wa utoaji haki kwa sehemu kubwa

ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka 2000. Nguzo tatu za maboresho zilizoimarishwa ni usimamizi bora wa rasilimali; upatikanaji na utoaji haki kwa wakati; na kudumisha imani ya jamii kwa mahakama na ushirikishaji wa wadau katika shughuli za mahakama.

Ili kufanikisha haya, Mhimili wa Mahakama, kupitia maboresho, umejenga na kutumia mifumo ya kisasa ya kiteknolojia pamoja na matumizi ya akili mnemba *(artificial intelligence)* katika mnyororo na mfumo mzima wa utoaji haki; kuongeza kubwa la rasilimaliwatu ikiwemo ajira za Mahakimu, na uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu.

Hata hivyo, juhudi hizi za kupata mafanikio makubwa Mhimili wa Mahakama umeendelea kukabiliwa na vikwazo mbalimbali vikiwemo uhaba na uchakavu wa majengo katika ngazi zote za Mahakama.

**Mheshimiwa Rais, Mahakama ya Tanzania ilihitaji mabadiliko makubwa ya kifikra na kimtizamo ili itekeleze Dira ya Mwaka 2025 kupitia Mpangomkakati na Programu za Maboresho.**

Maboresho endelevu yanahitaji kubadili mitazamo na tamaduni *(mindsets)* katika utoaji huduma. Hivi sasa watumishi wa Mahakama wanafanya kazi kwa kuleta matokeo yanayopimika na kwa kuzingatia uweledi *(professionalism).* Watumishi wa Mahakama wanafanya kazi kwa ushirikiano, mawasiliano, na kwa mashauriano. Utumishi wa Mahakama unalenga kutoa huduma zinazowaridhisha wadau, wadaawa, na watu wote wanaofuata huduma za Mahakama.

Hii ndiyo sababu kila baada ya miaka mitatu au minne, tangu mwaka 2015, Mahakama imekuwa ikifanya tathmini ya mara kwa mara kupitia tafiti maarufu zijulikanao kama TAFITI KUHUSU KIWANGO CHA KURIDHIKA KWA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA MAHAKAMA. Hadi sasa tafiti tatu zimefanyika (miaka 2015, 2019, na 2023). Kukubali kutathminiwa na kujitathmini kunahitaji mabadiliko makubwa ya kifikra.

**Mheshimiwa Rais,** kipekee nikushukuru sana, wewe binafsi, pamoja na Serikali unayoiongoza kwa kuwezesha mafaniko yote niliyoyataja hapo juu kupitia fedha za ndani

na za wahisani. Kwa utashi wako uliridhia na kufanikisha Serikali kuingia makubaliano na Benki ya Dunia kupata fedha za kutekeleza awamu ya kwanza na ya pili ya mradi wa maboresho uliomlenga mwananchi *(Citizen-Centric Judicial Modernization and Justice Service Delivery Project).* Kwa mujibu wa ripoti ya utafiti uliofanywa na taasisi isiyo ya kiserikali ya REPOA *(REPOA Court Users' Survey Reports - 2015, 2019 & 2023)*, kumekuwa na mafanikio ambayo yamejidhihirisha katika maeneo mengi ikiwemo ukuaji wa kuridhika kwa watumiaji wa huduma za mahakama kutoka asilimia **61** mwaka **2015** hadi asilimia **78** mwaka **2019**, na asilimia **88** mwaka **2023.**

## 3. TAASISI ZA HAKI-MADAI NA MALENGO YA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO YA MWAKA 2050

**Mheshimiwa Rais**, kama tunavyojua, taifa liko katika maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050. Rasimu ya Dira hii imesambazwa kwa wananchi kwa ajili ya kutoa maoni. Kwa mwaka huu 2025, Wiki na Siku ya Sheria Tanzania imetumika kama fursa adhimu kuhakikisha kuwa maoni ya taasisi za haki-madai yanatolewa kikamilifu ili kuwezesha upatikanani wa Dira ya Mwaka 2050 itakayotumika kama kichocheo cha uboreshaji wa huduma za utoaji haki. Umuhimu wa Dira ya Mwaka 2050 si tu kwa taasisi za haki-madai, bali ni muhimu kwa taasisi zote za utoaji haki na wananchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Rais,** katika kuelekea Tanzania ya Mwaka 2050, taasisi za hakimadai zina nafasi ya kipekee katika kuhakikisha malengo ya maendeleo ya taifa yanafikiwa. Taasisi hizi ni pamoja na Mahakama ya Tanzania; Tume ya Utumishi wa Mahakama; Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA); Wizara ya Katiba na Sheria; Tume ya

Kurekebisha Sheria; Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS); na taasisi zingine ambazo, kwa namna moja au nyingine, zinahusika na haki-madai bila kuwasahau wananchi wote.

**Mheshimiwa Rais,** kutokana na uzoefu wake katika kutumia Dira ya Mwaka 2025 kufanya maboresho yake, Mahakama ya Tanzania itaipokea Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2050 kama kielelezo cha utashi wa kisiasa kwa taasisi zinazosimamia haki-madai na zile zinazosimamia haki-jinai kuwa zinatakiwa kufanya mabadiliko makubwa ili zifanikishe Taifa kufikia malengo na matarajio ya Dira ya Mwaka 2050.

**Mheshimiwa Rais,** kufikiwa kwa Malengo ya Dira ya Mwaka 2050, kwa kiasi kikubwa, kutategemea mabadiliko makubwa yatakayofanywa ndani ya taasisi zinazosimamia haki-madai ili ziwezeshe Tanzania kufikia maono na dhamira ya kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu au juu zaidi. Taasisi zinazosimamia haki-madai ndizo zinategemewa kuwa watekelezaji wakubwa wa ramani ya mabadiliko ya taifa itakayowekwa na Dira ya Mwaka 2050.

Kukuza utajiri ili kuongeza viwango vya ubora wa maisha na kutokomeza umaskini hakuwezi kufanikiwa endapo taasisi za umma zitashindwa kufanya mabadiliko ya ndani ya taasisi. Ndoto ya jamii ya Watanzania kuwa yenye ustawi, usawa, na kujitosheleza haiwezekani bila ya taasisi za umma kufanya mabadiliko makubwa ya ndani na kuwa na mwelekeo wa kutekeleza Dira ya Mwaka 2050.

Tanzania ya Dira ya Mwaka 2050 haiwezi kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la idadi ya watu bila taasisi husika na maeneo hayo kubadilika kutoka mazoea ya sasa. Aidha, Tanzania ya Dira ya Mwaka 2050 haiwezi kufaidi matunda ya matumizi ya teknolojia za habari na mawasiliano hususani akili mnemba bila kufanya mabadiliko makubwa katika taasisi husika na kuziweka kwenye utayari.

## 4. NAFASI YA TAASISI ZA HAKI-MADAI KATIKA KUFIKIA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO YA MWAKA 2050

**Mheshimiwa Rais**, taasisi za haki-madai ni vyombo vinavyohusika na mchakato wa utungaji wa sheria zinazohusiana na mashauri ya madai, usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai, na utoaji wa haki-madai. Kwa uhalisia, tafsiri ya "taasisi zinazosimamia haki-madai" ni pana zaidi ya Mahakama na wadau wake walio katika mnyororo wa utoaji haki unaoishia mahakamani. Zipo taasisi zingine ambazo huduma zao zinagusa haki-madai za wananchi kila siku na ambazo zinahitaji kufanyiwa mabadiliko makubwa ili ziweze kuifikisha Tanzania katika uchumi wa kati ngazi ya juu.

Mifano ya taasisi hizi ni pamoja zile zinazosimamia ardhi, maji, misitu, hifadhi, madini, leseni, na vibali mbalimbali ambazo kila siku zinagusa haki za wananchi.

Mathalani, taasisi zinazohusika na ardhi zikifanya usimamizi endelevu wa ardhi, migogoro mingi ya ardhi itaishia kwenye usuluhishi bila kufikishwa mahakamani.

**Mheshimiwa Rais, usimamizi endelevu wa ardhi ni mtaji muhimu wa kufikia malengo na matarajio ya Dira ya Mwaka 2050:**

Aya ya 4.3.4 katika rasimu ya Dira ya Mwaka 2050 inahusu usimamizi endelevu wa ardhi, eneo ambalo linasimamiwa na taasisi tofauti-tofauti na sheria mbalimbali zinazogusa haki mbalimbali za wananchi. Taasisi hizi zilizopewa majukumu ya usimamizi endelevu wa ardhi zinatakiwa kujipanga sasa na si kesho, ili ziwe na utayari wa kukabiliana na kasi ya ongezeko la idadi ya watu, ukuaji wa miji, upanuzi wa shughuli za kilimo, uchimbaji madini, na maendeleo ya viwanda yatakayoongeza uhitaji mkubwa wa rasilimali za ardhi, hivyo kuleta uwezekano wa kuibuka kwa migogoro itakayohitaji utatuzi wa haraka.

Taasisi zinazohusika na usimamizi endelevu wa ardhi zisipojipanga, badala ya kuchochea ukuaji wa uchumi endelevu, zitakuwa vyanzo vya migogoro ya ardhi itakayolundikana katika ngazi mbalimbali za mahakama.

## MAENEO YA HAKI-MADAI YALIYOUNDIWA TUME YA RAIS

**Mheshimiwa Rais,** kuna maeneo mengi ambayo wewe binafsi umeonesha dhamira ya kutaka mabadiliko makubwa ya taasisi zinazosimamia haki-madai ili kukidhi matakwa ya safari ya kufikia Tanzania ya uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu au juu zaidi, uchumi unaokua kwa kasi na unaoimarisha ustawi wa watu kwa kuboresha huduma za jamii na kupunguza umaskini.

Kwa mfano, hakuna shaka yoyote kuwa, Tume ya Rais ya Kutathmini na Kushauri Masuala ya Kodi itakapokamilisha kazi yake, itasababisha mabadiliko makubwa katika taasisi mbalimbali zinazosimamia haki-madai. Mwelekeo huu wa mabadiliko makubwa yanayotarajiwa, yalibainishwa katika nukuu kutoka katika Taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais - Ikulu kwa vyombo vya habari ya tarehe 04 Oktoba 2024 isemayo *"Tume hiyo imeundwa kwa lengo la kufanya tathmini ya mfumo mzima wa kodi, kuimarisha zaidi mfumo huo, na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kurahisisha usimamizi wa ukusanyaji wa kodi nchini.... Pia,*

*amesisitiza umuhimu wa nchi kuwa na mfumo wa kodi unaochochea ukuaji uchumi wa viwanda na kuchangia ujenzi wa uchumi jumuishi, unaoiwezesha Serikali kuwa na vyanzo vya uhakika na vinavyotabirika ili kuleta ustawi wa wananchi".*

**Mheshimiwa Rais,** lugha uliyoitumia wakati unaizindua Tume ya Rais ya Masuala ya Kodi ni lugha ya DIRA ya Mwaka 2050, ni lugha inayozitaka taasisi zote zinazosimamia haki-madai na haki-jinai zitathmini mifumo, sheria, na taratibu zao za utoaji huduma ili ziweze kuchochea ukuaji wa uchumi na kufikia malengo ya Dira ya Mwaka 2050 ya uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu au juu zaidi, utakaokua kwa kasi, na utakaoimarisha ustawi wa watu kwa kuboresha huduma za jamii na kupunguza umaskini.

**Mheshimiwa Rais,** kuna usemi kuwa, "Mvaaji wa viatu ndiye anayejua wapi kiatu chake kinabana". Taasisi za umma na taasisi za haki-madai tunatakiwa kuanza kujua maeneo yanayohitaji mabadiliko na maboresho makubwa ili ziweze kwenda kasi ya kufikia malengo na matarajio ya Dira ya Mwaka 2050.

Taasisi zinazosimamia haki-madai zina jukumu la kuchangia kikamilifu upatikanaji wa dira itakayoboresha huduma za utoaji haki na zina wajibu wa kuweka mikakati thabiti ya kuwezesha utekelezaji wa Dira ya Mwaka 2050.

Kwa kutumia sitiari hiyohiyo ya mvaa viatu kufahamu wapi kiatu kinabana, Mahakama inafahamu vyema kuwa mashauri yaliyoko mbele yake yameshikilia rasilimali, milki za ardhi, hisa, muda, na fedha ambazo ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi. Mahakama inafahamu kuwa umalizikaji kwa haraka wa migogoro huwezesha rasilimali hizo kutumika kwa ufanisi mkubwa. Kwa kuzingatia ukweli huo, Mahakama imekuwa ikiyapigia chapuo mabadiliko ya mara kwa mara ya mifumo ya kidigitali na kutumia vyema fursa za mifumo ya kidigitali kwa kutoa huduma zake za utoaji haki kwa wakati na haraka kwa kutumia teknolojia za habari na mawasiliano. Aidha, Mahakama imedhamiria kuendelea kuboresha huduma zake kwa kwenda sambamba na mabadiliko ya mara kwa mara ya kiTEHAMA kwa kuwashirikisha wadau wote wa haki-jinai na haki-madai.

**Mheshimiwa Rais,** mafanikio ya Mahakama ya kutumia

mifumo ya kidigitali kutoa huduma zake yataisaidia Mahakama kumudu kasi ya mabadiliko yanayotarajiwa wakati wa utekelezwaji wa Dira ya Mwaka 2050. Katika kufanya mabadiliko makubwa yanayotarajiwa na Dira, taasisi za haki-madai haziwezi kuepuka matumizi ya teknolojia na hususani akili mnemba. Katika dunia, ambayo teknolojia, hususani matumizi ya akili mnemba, zinabadilika kwa kasi kubwa, taasisi zinazosimamia haki-madai haziwezi kusaidia Tanzania kufikia uchumi wa nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu au juu zaidi endapo zitaachwa nyuma katika matumizi hayo ya teknolojia na akili mnemba.

## DIRA YA MWAKA 2050 INAZITAKA TAASISI ZA HAKI-MADAI KUFANYA MABADILIKO MAKUBWA

**Mheshimiwa Rais,** safari ya Tanzania kuelekea kuwa nchi yenye uchumi wa kati daraja la juu kwa mujibu wa Dira ya Mwaka 2050 si sawa na matembezi ya kujistarehesha bustanini *(It will not be like a walk in the park)*. Nahau hii inatukumbusha kuwa mabadiliko makubwa yanayotarajiwa na Dira ya Mwaka 2050 ni safari inayohitaji matayarisho ya kina miongoni mwa taasisi zote za umma zinazotarajiwa

kufanya mabadiliko makubwa.

Kwa mujibu wa kaulimbiu ya Wiki na Siku ya Sheria Tanzania mwaka huu, 2025 ni mwaka wa taasisi zinazosimamia haki-madai kujiangalia na kutathmini taratibu na ngazi zao mbalimbali zilizopo ambazo hupitiwa kabla ya huduma kumfikia mlengwa. Ni wakati wa kutambua kwa kina mchakato wa msingi wa uendeshaji wa shughuli zao *(Core Business Process)* ili kujua mabadiliko wanayopaswa kuyafanywa ili taasisi zao ziweze kutekeleza Dira ya Mwaka 2050. Mabadiliko ya kitaasisi yanayohitajika kufanikisha Dira ya Mwaka 2050 yanahitaji kila taasisi peke yake au kwa kushirikiana na taasisi zingine kujiwekea mikakati ya kuchakata upya taratibu zao na ngazi mbalimbali za kutoa huduma *(Business Process Rengineering—BPR)* kwa faida ya ufanisi katika utoaji wa huduma za taasisi hiyo.

**Mheshimiwa Rais,**

Kabla sijahitimisha hotuba yangu na kukukaribisha, ninaomba nigusie mapendekezo ya maboresho ya maslahi ya watumishi wa mahakama yaliyowasilishwa

kwako na Tume ya Utumishi wa Mahakama, ambayo Jaji Mkuu ni mwenyekiti na Serikali ikaanza kuyafanyia kazi. Nichukue fursa hii kukushukuru kwa jinsi ambavyo Serikali unayoiongoza inaendelea kushughulikia maslahi ya watumishi wa Mahakama. Mtendaji Mkuu wa Mahakama amenijulisha kuwa amefahamishwa na Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi kuwa kuna maboresho mengine ya posho yamekamilika. Ninatanguliza shukrani za dhati kabisa kwa jitihada zako hizi na za Serikali unayoiongoza.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Rais,**

Mwisho kabisa ninakushukuru tena Mhe. Rais kwa kukubali kutenga muda wako kuhudhuria na kuwa mgeni rasmi katika siku hii muhimu. Niwashukuru pia wananchi wote waliojitokeza kwenye wiki ya elimu ya sheria. Nina imani kubwa kuwa wamejifunza mambo mengi yahusuyo Mahakama na wadau wake. Ninawahakikishia kuwa maoni tuliyoyapokea yatakuwa ngazi ya kupanda kuelekea katika maboresho zaidi ya shughuli zetu za utoaji huduma za

kimahakama.

**Mheshimiwa Rais,** sasa nikuombe utufanyie mambo mawili makubwa ambayo wadau wa sheria na Watanzania kwa ujumla wanasubiri kwa shauku kubwa; yaani kuhutubia hadhara hii ambapo utakuwa anaongea na Taifa kwa ujumla kupitia vyombo vya habari; na la pili ni kutuzindulia mwaka wa kazi wa kimahakama kwa mwaka 2025.

***Mhe. Rais, karibu sana!***

***ASANTENI KWA KUNISIKILIZA!***


# MUHTASARI WA TAARIFA YA SHUGHULI ZA KIMAHAKAMA KWA MWAKA 2024.

## 1. UTANGULIZI

Taarifa hii inatoa muhtasari wa hali ya mashauri katika kipindi cha mwaka 2024, ikijumuisha idadi ya mashauri yaliyofunguliwa, yaliyosikilizwa na kumalizika, pamoja na yale yaliyobaki katika ngazi zote za Mahakama kufikia tarehe 31 Disemba,2024. Taarifa hii pia inaonyesha hali ya mlundikano wa mashauri, huduma ya Mahakama Inayotembea, matumizi ya TEHAMA katika usikilizaji wa mashauri pamoja na usimamizi na ukaguzi wa Mahakama na Magereza. Taarifa ya kina ya shughuli za kimahakama inaonyeshwa kwenye Ripoti ya Jumla ya Ufanisi Katika Utendaji Kazi za Kimahakama – 2024.


## 2. MASHAURI YALIYOFUNGULIWA

Kwa mwaka 2024, jumla ya mashauri **242,284** yalifunguliwa katika ngazi zote za mahakama ikilinganishwa na mashauri **249,846** yaliyofunguliwa mwaka 2023. Hii inaonyesha punguzo la **3%.**




### 3. MASHAURI YALIYOSIKILIZWA NA KUMALIZIKA

Katika kipindi cha mwaka 2024, mashauri **245,310** yalisikilizwa na kumalizika. Hii ni sawa na asilimia **101** ya mashauri yaliyofunguliwa kwa mwaka 2024 na asilimia **84** ya mashauri yote yaliyokuwa mahakamani mwaka huo (yaliyofunguliwa mwaka 2024 na yaliyobaki 2023). Viwango vya umalizaji na uondoshaji wa mashauri vimeongezeka kwa asilimia **1** ikilinganishwa na mwaka 2023. Takwimu hizi zinaashiria ongezeko la ufanisi wa usikilizaji wa mashauri.




## 4. MASHAURI YALIYOBAKI

Kwa ngazi zote za Mahakama yalibaki mashauri **43,992** ikiwa ni pungufu la mashauri **7,338** ikilinganishwa na mashauri yaliyobaki mwaka 2023. Aidha, kumekuwa na mafanikio makubwa katika Mahakama za Mwanzo ambapo Mahakama za Mwanzo **299** zimemaliza mwaka zikiwa hazina mashauri kabisa.

Hali ya ufunguaji, usikilizaji na bakaa ya mashauri kwa ngazi zote ni kama ifuatavyo:

| NGAZI YA MAHAKAMA | YALIYOFUNGULIWA | YALIYOISHA | YALIYOBAKI |
|---|---|---|---|
| Mahakama ya Rufani | 3,094 | 2,095 | 6,203 |
| **Jumla Ndogo** | **3,094** | **2,095** | **6,203** |
| Masjala za Mahakama Kuu | 16,738 | 17,707 | 9,556 |
| Divisheni ya Biashara | 929 | 792 | 418 |
| Divisheni ya Ardhi | 2,143 | 2,458 | 791 |
| Divisheni ya Kazi | 1,277 | 1,296 | 319 |
| Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi | 170 | 157 | 57 |
| **Jumla Ndogo-Divisheni** | **4,519** | **4,703** | **1,585** |
| **Jumla Ndogo Mahakama Kuu** | **21,257** | **22,410** | **11,141** |
| Mahakama za Hakimu Mkazi | 5,640 | 6,150 | 2,237 |
| Mahakama za Wilaya | 39,526 | 40,644 | 13,438 |
| Mahakama za Watoto | 1,443 | 1,510 | 349 |
| **Jumla Ndogo** | **46,609** | **48,304** | **15,591** |
| Mahakama za Mwanzo | 171,324 | 172,501 | 10,624 |
| **JUMLA KUU** | **242,284** | **245,310** | **43,992** |

Aidha, jedwali hapa chini linaonyesha mchango wa kila ngazi ya Mahakama katika ufunguaji na usikilizaji wa mashauri pamoja na kiwango cha umalizaji wa mashauri. Takwimu zinaonyesha kuwa ngazi zote za Mahakama, isipokuwa Mahakama ya Rufani, zimemaliza mashauri mengi zaidi ya yale yaliyofunguliwa na hivyo kutotengeneza mlundikano wa mashauri. Aidha, Mahakama Kuu Kituo cha Usuluhishi ambacho kinasuluhisha mashauri ya Mahakama Kuu Masjala ya Dar es Salaam na Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi kimesuluhisha mashauri **358** ambapo mashauri 107 kati ya hayo usuluhishi wake ulifanikiwa.

Kama ilivyokuwa mwaka 2023, mwaka 2024 Mahakama za Mwanzo zilipokea na kumaliza asilimia **71** na **70** mtawalia ya mashauri yote yaliyopokelewa na kumalizika katika Mahakama za ngazi zote nchini.

| Ngazi ya Mahakama | Yaliyofunguliwa | Yaliyoisha | Yaliyobaki | Wastani wa Mashauri kwa Jopo/Jaji /Hakimu | % ya Yaliyofunguliwa | % ya Yaliyomalizika | Kiwango cha Umalizaji wa Mashauri |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahakama ya Rufani | 3,094 | 2,095 | 6,203 | 754 | 1 | 1 | 68 |
| Mahakama Kuu | 21,257 | 22,410 | 11,141 | 332 | 9 | 9 | 105 |
| Mahakama za Hakimu Mkazi | 5,640 | 6,150 | 2,237 | 139 | 2 | 3 | 109 |
| Mahakama za Wilaya | 39,526 | 40,644 | 13,438 | 185 | 16 | 17 | 103 |
| Mahakama za Watoto | 1,443 | 1,510 | 349 | 7 | 1 | 1 | 105 |
| Mahakama za Mwanzo | 171,324 | 172,501 | 10,624 | 229 | 71 | 70 | 101 |
| **Jumla** | **242,284** | **245,310** | **43,992** | **229** | **100** | **100** | **101** |

## 5. MLUNDIKANO WA MASHAURI

Shauri linachukuliwa kuwa ni la mlundikano endapo limekaa mahakamani kwa zaidi ya miaka miwili kwa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu, mwaka mmoja kwa Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya na miezi sita kwa Mahakama za Mwanzo.

Idadi ya mashauri ya mlundikano kwa mwaka 2024 ni **1,724** ikilinganishwa na mashauri **2,594** mwaka 2023 sawa na **4%** ya mashauri yaliyopo Mahakamani. Mlundikano wa mashauri umepungua kwa asilimia **1** ikilinganishwa na mwaka 2023. Jedwali hapa chini linaonyesha hali ya mlundikano kwa kila ngazi ya mahakama.

| Ngazi ya Mahakama | Mashauri ya Mlundikano 2023 | Mashauri ya Mlundikano 2024 | Tofauti Kati ya 2023 na 2024 | Hali ya Mlundikano |
|---|---|---|---|---|
| Mahakama ya Rufani | 1,159 | 1,273 | 114 | Umeongezeka. |
| Mahakama Kuu | 292 | 175 | 117 | Umepungua. |
| Mahakama za Hakimu Mkazi | 455 | 144 | 311 | Umepungua. |
| Mahakama za Wilaya | 664 | 126 | 538 | Umepungua. |
| Mahakama za Watoto | 18 | 0 | 18 | Umepungua. |
| Mahakama za Mwanzo | 6 | 6 | 0 | Umebaki kama ulivyokuwa. |
| **Jumla** | **2,594** | **1,724** | **1,098** | Umepungua |

Hali ya mlundikano wa mashauri katika kila ngazi ya Mahakama na asilimia inayochangia ni kama ifuatavyo: -

| Ngazi ya Mahakama | Mashauri yaliyobaki | Mashauri ya Mlundikano | % ya Mlundikano | % ya Mchango wa Mlundikano |
|---|---|---|---|---|
| Mahakama ya Rufani | 6,203 | 1,273 | 21% | 74% |
| Mahakama Kuu | 11,141 | 175 | 2% | 10% |
| Mahakama za Hakimu Mkazi | 2,237 | 144 | 6% | 8% |
| Mahakama za Wilaya | 13,438 | 126 | 1% | 7% |
| Mahakama za Watoto | 349 | 0 | 0% | 0% |
| Mahakama za Mwanzo | 10,624 | 6 | 0% | 0% |

## 6. HUDUMA YA MAHAKAMA INAYOTEMBEA

Kwa mwaka 2024 Mahakama imeongeza wigo wa huduma ya Mahakama Inayotembea baada ya kununua magari mawili na hema la haki moja. Hema na magari hayo yanatoa huduma katika mikoa ya Mbeya na Dodoma na hivi karibuni huduma zitaanza katika Mkoa wa Tabora.

Mahakama Inayotembea ilifunga mwaka 2023 ikiwa na mashauri 39. Mwaka 2024 mashauri 2,369 yalisajiliwa,

2,408 yakasikilizwa na kumalizika sawa na asilimia 99 ya mashauri yote yaliyosajiliwa. Mashauri yaliyobaki 2024 ni 34. Kwa mwaka 2024 pekee, huduma hii imewanufaisha watu **14,225** wakiwemo wanawake 7,697 na wanaume 6,528.

## 7. WASTANI WA MUDA ULIOTUMIKA KUTOKA KUFUNGULIWA KWA SHAURI HADI KUAMULIWA

Mahakama ina wajibu wa kutoa haki kwa wakati, hivyo muda ni muhimu katika utoaji haki. Kwa ujumla, katika mwaka 2024 muda wa wastani uliotumika kutoka kufunguliwa kwa shauri hadi kuamuliwa ulipungua hadi wastani wa siku 78 ikilinganishwa na siku 84 mwaka 2023. Mahakama za Mwanzo, ambazo zilihudumia asilimia 70 ya wananchi waliotafuta haki mahakamani, zilitumia wastani wa siku 37 kumaliza shauri.

## 8. MASHAURI YALIYOFUNGULIWA KWA WINGI

Kwa mwaka 2024, mashauri ya jinai yaliyofunguliwa kwa wingi mahakamani yalihusisha makosa ya usalama barabarani, ubakaji, madawa ya kulevya, mauaji na uhamiaji. Aidha kwa upande wa madai mashauri mengi yalihusisha

madai ya kawaida, ardhi, mirathi na madai yanayohusiana na watoto.

## 9. MATUMIZI YA TEHAMA KATIKA UTOAJI HAKI

Mahakama imeendelea kutumia mifumo ya TEHAMA katika utoaji haki ikiwemo Mfumo wa Usimamizi wa Mashauri (JoT e-CMS), Mfumo wa Kunukuu na Kutafsiri Mwenendo wa Mashauri (TTS), Mfumo wa Takwimu (Data Hub), Mfumo wa Usimamizi wa Mawakili (e-Wakili), Mfumo wa Maktaba Mtandao, Mfumo wa Taarifa za Hukumu na Sheria Tanzania (TanzLII), Virtual Court n.k. Mifumo hii imeendelea kuongeza ufanisi na uwazi katika usajili na usikilizaji wa mashauri pamoja na uzalishaji wa taarifa za mashauri.

Usikilizaji wa mashauri kwa njia ya mtandao uliiwezesha Mahakama kusikiliza mashauri yaliyowahusisha mashahidi na wadaawa kutoka ndani na nje ya nchi ikiwemo Oman, Iraq, Jordan, Uingereza, Ujerumani, India, Marekani, Uganda na Iran.

Aidha kwa mwaka 2024, jumla ya maamuzi 6,671 yalichapishwa kwenye maktaba mtandao baada ya

maamuzi hayo kutolewa kwenye JoT e-CMS. Aidha, jumla ya maamuzi 60,319 yamechapishwa katika mfumo wa TanzLII toka kuanzishwa kwake na kwa mwaka 2024 pekee, mashauri 10,795 yalipandishwa kwenye mfumo huo. Aidha, upatikanaji wa huduma ya TanzLII bila mtandao (Pocket Law) pamoja na sheria mbalimbali, ambao ni matokeo ya ushirikiano kati ya Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mwandishi Mkuu wa Serikali, umeifanya TanzLII kuwa mfumo wa taarifa za hukumu na sheria unaotembelewa zaidi ulimwenguni kwa miaka mitano mfululizo.

## 10. USIMAMIZI NA UKAGUZI WA MAHAKAMA NA MAGEREZA

- **Ukaguzi wa Mahakama**

Katika mwaka 2024, ukaguzi wa huduma za Mahakama ulifanyika kwa lengo la kuhakikisha ubora wa huduma zinazotolewa na Mahakama. **Kiwango cha ukaguzi kimeongezeka kwa asilimia 1.75,** kutoka asilimia **98.1** mwaka 2023 hadi asilimia **99.7** mwaka 2024. Matokeo ya ukaguzi yanaonesha kupungua kwa changamoto zinazojirudia,

kupungua vituo vyenye changamoto na Mahakama zenye mashauri ya mlundikano. Ufanisi uliopatikana ni matokeo ya Uimarishaji wa Usimamizi na Ukaguzi wa Mahakama, Mafunzo, Uboreshaji wa Miundombinu na ongezeko la matumizi ya TEHAMA.

- **Ukaguzi wa Magereza**

Kwa Kipindi cha Jan-Des, 2024 ukaguzi ulifanyika katika robo zote nne za mwaka ambapo magereza yalikaguliwa kwa wastani wa 75.2%, hii ikiwa ni sawa ongezeko la 11.7% ikilinganishwa na wastani wa kiwango cha ukaguzi mwaka 2023 ambapo ukaguzi ulifanyika kwa wastani wa 63.5%.





Taarifa zinabainisha kupungua kwa idadi ya wafungwa na mahabusu kwa baadhi ya magereza ingawa bado kuna uwepo wa idadi kubwa ya wafungwa na mahabusu inayozidi uwezo wa baadhi ya Magereza. Magereza hayo ni pamoja

na Ukonga, Segerea, Keko, Shinyanga, Tarime, Morogoro, Mpanda, Ruanda, Tukuyu, Isanga na Bangwe.

## 11. MAAFISA MAHAKAMA

Mwaka 2024 aliteuliwa Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufani hivyo kufanya idadi ya Majaji wa Mahakama hiyo kufikia 36. Aidha Majaji watano wa Mahakama Kuu waliteuliwa. Uteuzi huu ulifanya majaji wa Mahakama Kuu kufikia 110. Katika kipindi hicho pia aliteuliwa Msajili Mkuu, Msajili wa Mahakama ya Rufani na Msajili wa Mahakama Kuu. Naibu Wasajili sita nao waliteuliwa na kufanya idadi ya Wasajili na Naibu Wasajili kufikia 83. Uteuzi mwingine ulihusisha Mahakimu Wafawidhi wa Mikoa sita na wa Wilaya watatu. Aidha, Mahakimu Wakazi 86 waliajiriwa na hivyo kuongeza idadi ya Mahakimu Wakazi hadi 1,228. Hadi mwishoni mwa mwaka, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo yaani PCM walikuwa 196 hivyo, jumla ya Mahakimu wote ni 1424. Idadi ya Maafisa Mahakama kwa jinsia ni kama inavyoonekana kwenye jedwali.




Aidha, kwa mwaka 2024 Maafisa wa Mahakama 20 walikoma utumishi wa Mahakama kwa sababu mbalimbali; watatu waliacha kazi, 12 waliachishwa kazi na wengine watano waliaga dunia. Wapendwa wetu tuliowapoteza ni Mhe Mwanaisha Athuman Kwariko, Jaji wa Mahakama ya Rufani; Mhe, Maximilian Alphonce Malewo, Naibu Msajili; Mhe. Bridget Mathew Sengwaji, Hakimu Mkazi Mkuu; Mhe Batista Kindaga Kashusha, Hakimu Mkazi Mfawidhi (W) Masasi; na Mhe. Mwajuma Issa Lembuya, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Mkuu. Roho zote za marehemu wapendwa wetu zipate pumziko la Amani.

THE JUDICIARY OF TANZANIA

MAHAKAMA YA TANZANIA

Mahakama ya Tanzania